

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
OFISI YA RAIS  
TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA



OFISI YA MKUU WA MKOA  
KIGOMA

S.L.P 125, KIGOMA, Simu: 028-280-2330, Fax: 028-280-2330/4444, E-mail:ras@kigoma.go.tz

Tarehe: 11 Oktoba, 2022

---

**TAARIFA KWA UMMA**

**YAH: ZIARA YA MHE. SAMIA SULUH HASSAN RAIS WA JAMHURI YA  
MUUNGANO WA TANZANIA**

Mhe. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania, anatarajia kufanya Ziara ya Kikazi ya siku Nne (4) Mkoani Kigoma kuanzia Siku ya tarehe 16 hadi tarehe 19 Oktoba, 2022.

Akizungumza na Waandishi wa Habari na Viongozi Taasisi mbalimbali Mkoani Kigoma Mkuu wa Mkoa wa Kigoma Kamishna Jenerali Mstaafu wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji Mhe. Thobias Emir Andengenye amesema Mhe. Rais anatarajiwa kuwasili Mkoani Kigoma **Siku ya tarehe 16 hadi 19 Oktoba, 2022**, ambapo atapokelewa katika Wialaya ya Kakonko majira ya **Saa 4:00 Asubuhi**. Mhe. Rais, akiwa Mkoani Kigoma atatembelea Wilaya ya, **Kakonko, Kibondo, Kasulu, Buhigwe, Kigoma, na Uvinza**.

Akiwa Mkoani Kigoma Mhe. Rais atafungua na kuweka mawe ya msingi katika miradi na atazindua miradi ya Afya, Maji, Barabara na kukagua shughuli mbalimbali za maendeleo Mkoani Kigoma. Aidha, Mhe. Rais

atapata fursa ya kuzungumza na Wananchi katika maeneo mbalimbali ya Wilaya atakazopita.

Hii ni ziara yake ya kwanza Mkoani kwetu tangu aingie madarakani. Kwetu sisi wanakigoma ni faraja kubwa kumpokea Rais wetu, kwa furaha kabisa tujitokeze kumlaki. Mkuu wa Mkoa amewataka Wananchi wa Mkoa wa Kigoma, kujitokeza kwa wingi kumpokea na kumlaki Kiongozi wetu wa Kitaifa katika maeneo mbalimbali ambayo atatembelea na kuzungumza na Wananchi.



Andrew Mlama  
Afisa Habari  
Sekretarieti ya Mkoa  
**KIGOMA**